AZIMIO LA KAZI GREDI YA TISA (KISWAHILI)

JINA LA MWALIMU:____

SHULE:_______________________________MUHULA:______MWAKA:_________

Wk	KIP	MADA KUU	MADA NDOGO	MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA	MASWALI DADISI	SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI	NYENZO	TATHMINI	MAONI
1	1	**USALAMA BARABARANI Kuandika**	Insha za Kubuni Methali	Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya insha za methali ili kuipambanua, b) kujadili vipengele vya insha ya methali, c) kufurahia kufasiri methali na kuziandikia insha zinazoafiki ili kujenga ubunifu.	Unahitaji kufanya nini unapoandika insha ya methali?	Mwanafunzi aelekezwe: •kueleza maana ya insha za methali, •kusoma kielelezo cha insha ya methali, •kujadili na wenzake vipengele vya insha ya methali katika kielelezo cha insha aliyosoma,	Picha, Chati Michoro na picha KLB Top Scholar Kisw Gredi ya 9 Mwongozo wa mwalimu Uk. 68-70 KLB Top Scholar Kisw Gredi ya 9 Ktb cha mwanafunzi Uk.68-70	Kielelezo cha insha ya shajara	
	2		Insha za Kubuni Methali	Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze: a) kueleza maana ya insha za methali ili kuipambanua, b) kuandika insha ya methali kwa kuzingatia vipengele vya uandishi husika, c) kufurahia kufasiri methali na kuziandikia insha zinazoafiki ili kujenga ubunifu.	Unahitaji kufanya nini unapoandika insha ya methali?	Mwanafunzi aelekezwe: •kuandika insha ya methali (k.v. kuhusu methali zinazoangazia usalama barabarani; haraka haraka haina baraka, msafiri ni aliye pwani, polepole ndio mwendo) kwa kuzingatia vipengele vya uandishi wa insha ya methali. •kuwasomea wenzake insha aliyoandika ili waitolee maoni.	Picha, Chati Michoro na picha KLB Top Scholar Kisw Gredi ya 9 Mwongozo wa mwalimu Uk. 68-70 KLB Top Scholar Kisw Gredi ya 9 Ktb cha mwanafunzi Uk.68-70	Kielelezo cha insha ya masimulizi	

	3	**Sarufi**	Vielezi •Vielezi vya namna •Vielezi vya wakati	Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze: a) kutambua vielezi vya namna na vya wakati katika matini, b) kutumia vielezi vya namna na vya wakati ipasavyo katika matini, c) kuchangamkia kutumia vielezi vya namna na vya wakati katika matini.	1. Ni vielezi vipi unavyovijua? 2. Vielezi huchangia a vipi katika mawasiliano?	Mwanafunzi aelekezwe: •kuchopoa vielezi vya namna na vya wakati kutoka kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno au tarakilishi, •kuvipigia mstari vielezi vya namna na vya wakati katika sentensi na vifungu,	•Kapu maneno •Kadi maneno •Picha za vitu mbalimbali •Michoro, Chati KLB Top Scholar Kisw Gredi ya 9 Mwongozo wa mwalimu Uk. 70-73 KLB Top Scholar Kisw Gredi ya 9 Ktb cha mwanafunzi Uk.70-74	a) Kutambua k.m. kwenye orodha b) Kujaza mapengo c) Kutunga sentensi d)Kazi mradi	